BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 17 Juni, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

297. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni muda mrefu sana kisiwa cha Pemba kimekumbwa na tatizo sugu la kukosekana kwa gari la maji taka, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi pale ambapo magari haya yanapohitajika kuondoa maji taka katika maeneo mbali mbali.

(a) Je, ukweli wa suala hili unafahamika vipi na Wizara yako.

(b) Kwa kuwa tatizo hili ni la siku nyingi na lina umuhimu wake, je ni ipi hatua iliyochukuliwa na Serikali kuliondoa tatizo hili.

(c) Je, ni lini Wizara yako italiondoa tatizo hilo moja kwa moja.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

8. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

   Kifungu cha 210 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kimeelezea kuwa, Serikali itatoa ajira 300,000 kwa vijana wa Zanzibar ili kuwaondolea hali ngumu ya maisha yao.

   (a) Je, ni vijana wangapi hadi sasa wamepatiwa ajira hizo kama ambavyo zimeelezwa kwenye Ilani hiyo.

   (b) Kwa kuwa Zanzibar imegawia kimkoa na kwa kuwa katika kila Mkoa kuna vijana wengi wanaozurura mitaani, je, kila Mkoa umepata nafasi ngapi za ajira kati ya ajira zilizotolewa.

   (c) Je, ni upi mkakati mahasusi utakaochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha ajira zinapatikana kwa vijana kama zilivyoahidiwa.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

74. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Serikali inawahamasisha wananchi juu ya matumizi ya benki na kuwataka kuweka fedha zao na kuzitumia kupitia benki mbali mbali nchini.

    Kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma bora za kibenki bila ya kupata usumbufu wowote.

220. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

     Tathmini ya mwamko na uelewa wa wananchi katika uwekezaji wa soko la kifedha kupitia SUKUK ukoje kwa sasa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

16. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Timu za Tanzania bara za Simba, Yanga na Azam zimepiga hatua kubwa sana katika mashindano mbali mbali ya ndani na ya kimataifa kutokana na ufadhili na uwezeshwaji mkubwa unaofanywa na matajiri na wadhamini mbali mbali ambao wamejikita kuwekeza kwenye michezo.

    (a) Ni upi mkakati madhubuti unaofanywa na Serikali yetu wa kuzitafutia ufadhili kama huo timu zetu za Zanzibar.

    (b) Ni lini Serikali itaanza kufanya 'lobbing' kwa wawekezaji wetu waliopo ndani na nje ya nchi kuzisaidia timu zetu za Zanzibar.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

79. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

    Miongoni mwa wajibu wa Afisa Ustawi wa Jamii ni kushirikiana na Serikali za Mitaa katika kutoa ushauri na mafunzo kwa wazazi na walezi juu ya ustawi wa watoto.

    (a) Je, kwa namna gani suala hili limepewa uzito unaostahiki.

    (b) Mafanikio yepi yamepatikana katika utekelezaji wake.

    (c) Je, kuna changamoto gani zimejitokeza katika utekelezaji wake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

81. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Namba za nyumba na vibango vinavyowekwa barabarani ili kuonesha mitaa, ni sehemu ya kazi ya sensa na kujua idadi ya watu na makaazi kwa mwaka.

    Je, alama hizi ziliwekwa kwa utaratibu upi.

84. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni sababu zipi zinazopelekea ugumu wa kupatikana hati baada ya mafunzo ya udereva kwa wanaokwenda kutafuta huduma hii.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

284. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa ipo haja ya kuwa na Kalenda ya Kimasomo kwa Skuli za Msingi na Sekondari za hapa Zanzibar. Na kwa kuwa Kalenda hizo zitatoa nafasi zaidi kwa wanafunzi kuongeza siku za masomo kama ilivyo Tanzania bara na hususani kwa mwaka huu wa uchaguzi ili kuongeza ufaulu.

Je, Wizara yako imefikira vipi kulifanyia kazi suala hilo.

**Wizara ya Afya:**

47. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ugonjwa wa Mtoto wa Jicho unaonekana kuwa ni moja ya tatizo kubwa la ugonjwa wa macho linaloathiri wananchi wengi wa Zanzibar, na katika baadhi ya maeneo ya vijijini wengine ugonjwa huu huunasibisha na mambo ya kishirikina hivyo kupelekea athari zaidi kwa wagonjwa ambao huchelewa kupelekwa katika vituo vya afya.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inatambua kuwepo kwa ugonjwa huu.

(b) Je, Serikali imewahi kufanya tafiti juu ya chanzo cha ugonjwa huu wa Mtoto wa Jicho.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata tiba na kuutokomeza ugonjwa huu hatari.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

82. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni upi mpango wa Serikali juu ya afya za wanachi kupitia kilimo hai na utumiaji wa mbolea.

196. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni jitihada gani kwa ujumla ambazo wadau mbali mbali wamekuwa wakizifanya katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo.

198. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Ni lini dunia huadhimisha siku ya wanyama pori duniani na vipi kauli mbiu huchangia uhifadhi na haki zao.

(b) Tathmini iko vipi kwa binadamu katika kutegemea rasilimali zinazotokana na wanyama pori.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

54. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Zipo hadithi za kuvutia kwa wenzetu wa Mwanza kwa kuwekeza katika vizimba vya kufugia samaki kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Moja ya yanayotajwa ni uwekezaji endelevu wenye kutunza mazingira na kuleta tija kubwa kwa wananchi wanaofanya shughuli zao za ufugaji wa samaki.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti juu ya ufugaji wa kutumia vizimba na uwezekano wa kutekelezeka hapa Zanzibar.

(b) Ikiwa ni ufugaji unaosifiwa sana na Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT), je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeangalia haja na uwezekano wa kuwekeza katika mradi huu kwa maendeleo ya uvuvi Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni yepi maelezo fasaha na ya uhakika ya historia ya Msikiti wa Malindi maarufu kama Msikiti wa Bamnara.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**17 Juni, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**